

OSORO G. MOGERE

**UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION**

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

UZAMILI WA SANAA (M.A)

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2003

EAST AFRICANA COLLECTION

MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia uhakiki wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya kifeministi Riwaya tulizozitumia kama sampuli katika uhakiki huu ni nne nazo ni *Asali Chungu* (1977) *Utengano* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990). Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza tumejadili, somo la utafiti, sababu za kulichagua na madhumuni. Maelezo kuhusu mipaka na upeo wa tasnifu pia yametolewa katika sura hii. Katika sura hii pia tumeyajadili yaliyoandikwa kuhusu mada na hatimaye tumeeleza matawi mbalimbali ya nadharia tuliyotumia.

Sura ya pili inahusu maudhui ya Kifeministi katika riwaya za *Asali Chungu* na *Utengano*. Tumetoa muhtasari wa riwaya hizi mbili, maudhui ya kisiasa, kielimu, kisheria, kiuchumi, malezi ya mtoto wa kike na pia mwanamke katika ndoa.

Sura ya tatu ni kama inaendelea kuyachunguza maudhui ya kifeministi lakini kwa kurejelea riwaya za *Kiza Katika Nuru* na *Tata za Asumini*. Mambo tuliyotazama ni pamoja na mwanamke na utamaduni, mwanamke kielimu mwanamke kisiasa na pia mwanamke kiuchumi.

Sura ya nne inashughulikia suala la usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za S.A Mohamed.

Sura ya tano ni hitimisho. Tumerejelea yale yote yaliyojadiliwa katika sura zote. Pia tumetoa maoni yetu na mapendekezo kuhusu kufanywa kwa utafuti zaidi.